JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU



# SERA YA TAIFA YA KUDHIBITI UKIMWI

Dodoma
Novemba, 2001

KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI, DAR ES SALAAM - TANZANIA

# SERA YA TAIFA
# YA
# KUDHIBITI UKIMWI

**YALIYOMO**


*Mada* *Ukurasa*

Yaliyomo iii
Vifupisho vii
Dibaji ix

**1.0. USULI** 1

1.1. Athari ya Virusi vya UKIMWI (VVU)/UKIMWI ....... 1

1.2. Virusi vya UKIMWI/UKIMWI na Umaskini ......... 1

1.3. Fedheha na Virusi vya UKIMWI/UKIMWI .......... 2

1.4. Ugharimiaji wa Shughuli za Kitaifa za kukabiliana na Virusi vya UKIMWI/UKIMWI ........................ 2

1.5. Msukumo wa Kisiasa, Kiserikali na Uongozi ......... 3

1.6. Haja ya kuwepo na Sera ya Taifa kuhusu Virusi vya UKIMWI/UKIMWI ........................................ 3

1.7. Kanuni zinazolinda Sera ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI 4

**2.0. HALI ILIVYO KUHUSU UKIMWI** ................................ 6

2.1. Hali halisi ilivyo sasa .......................................... 6

2.2. Jinsi UKIMWI unavyoenezwa .............................. 6

2.3. Hatari ya Maambukizo ya UKIMWI ....................... 6

**3.0. MALENGO MAKUU YA SERA** .................................. 8

3.1. Utangulizi ........................................................ 8

3.2. Madhumuni Mahususi ya Sera ............................ 8

a) Kuzuia Kuenea kwa Virusi vya UKIMWI/ UKIMWI ............. 8

b) Kupima Virusi vya UKIMWI .................................. 9

c) Huduma kwa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI/UKIMWI (PLHAs) .................................. 9

d) Dhima na Ugharimiaji Kisekta .................................. 10

e) Utafiti .................................. 10

f) Masuala ya Utungaji Sheria na Sheria .................................. 11

g) Madhumuni Mengine .................................. 11

**4.0. HAKI ZA WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI/ UKIMWI NA HAKI ZA WANANCHI KATIKA JAMII** ......... 12

4.1. Madhumuni .................................. 12

**5.0. KUZUIA KUENEA KWA UKIMWI KWA KUJAMIIANA** ....... 14

5.1. Madhumuni .................................. 14

5.2. Kwa Vijana Walioko Shuleni na Kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu .................................. 14

5.3. Kwa Vijana Walio nje ya Shule .................................. 15

5.4. Kwa Watu Wazima .................................. 15

5.5. Kwa Watu wenye wapenzi zaidi ya mmoja na wanaofanya Biashara ya Ngono .................................. 15

5.6. Kwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya .................................. 15

5.7. Kwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI/ UKIMWI .................................. 15

5.8. Vyombo vya Habari .................................. 16

5.9. Kushiriki kwa Jamii .................................. 16

5.10. Kondomu .................................. 16

5.11. Kukinga na Kusimamia Maambukizo ya Magonjwa ya Zinaa .................................. 16

5.12. Uambukizaji kwa njia ya damu na bidhaa za damu, viungo vya mwili na majimaji ya mwili ...... 17

5.13. Uambukizaji kwa tiba ya upasuaji na utogaji, na tiba ya meno .................................................... 18

a) Utumiaji wa vifaa vinavyotumiwa mara moja tu, vinavyotumiwa tena na tena, na kuumia kwa bahati mbaya ............................................. 18

b) Uelimishaji wa watu wanaotumia huduma za afya ........................................................... 19

5.14. Kuzuia uambukizo wa UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto (PMTCT) ................................ 19

a) Maambukizo kabla ya kujifungua ....................... 19

b) Maambukizo wakati wa kujifungua .................... 20

c) Maambukizo baada ya kujifungua ...................... 20

5.15. Masuala ya Jinsia kuhusiana na VVU/UKIMWI ..... 20

**6.0. KUPIMA Virusi Vya UKIMWI** ........................................ 22

6.1. Madhumuni ................................................... 22

6.2. Kupima VVU/UKIMWI ........................................... 22

6.3. Usiri ................................................................ 22

6.4. Ridhaa ya kutoa taarifa ...................................... 23

6.5. Kumtaarifu mpenzi .............................................. 23

6.6. Kumtia mtu hatiani kwa kosa la jinai kwa kuambukiza VVU kwa makusudi ....................................... 23

6.7. Kupima VVU kabla ya ndoa .................................. 23

6.8. Utafiti unaohusu upimaji wa VVU .......................... 24

6.9. Uchunguzi wa VVU .............................................. 24

6.10. Gharama za vipimo vya VVU................................. 24

6.11. Upimaji VVU wakati wa ujauzito .......................... 24

'.0. **HUDUMA KWA WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI** ........ 25

7.1. Madhumuni ........ 25

7.2. Huduma za Matunzo na Msaada vinavyotolewa na Jamii ........ 26

7.3. Kinga kwa Watoa huduma za Afya ........ 26

7.4. Huduma za Msaada ........ 27

:.0. **UTAFITI** ........ 28

8.1. Utangulizi ........ 28

8.2. Taratibu za utafiti kuhusu VVU/UKIMWI ........ 28

8.3. Vipaumbele vya utafiti wa Taifa kuhusu VVU/UKIMWI ... 29

8.4. Usambazaji wa matokeo ya Utafiti ........ 29

8.5. Ugharimiaji wa Utafiti wa VVU/UKIMWI ........ 29

·.0. **DHIMA ZA SEKTA NA UGHARIMIAJI** ........ 30

9.1. Madhumuni ........ 30

0.0. **MUUNDO WA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI (TACAIDS)** ........ 31

10.1. Utangulizi ........ 31

10.2. Dira ........ 31

10.3. Jukumu Maalumu ........ 31

10.4. Lengo ........ 31

10.5. Madhumuni ........ 31

10.6. Kazi za Tume ........ 32

10.7. Sera ........ 33

**VIFUPISHO**:

| | |
|---|---|
| AIDS: | Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) |
| ART: | Tiba ya Kusogeza mbele siku za kuishi |
| CBO: | Mashirika ya Kijumuiya |
| HAARD: | Dawa zenye nguvu sana za kusogeza mbele siku za kuishi |
| HAART: | Tiba yenye nguvu sana ya kusogeza mbele siku za kuishi |
| HIV: | Virusi vya UKIMWI (VVU) |
| IEC: | Habari, Elimu na Mawasiliano |
| ICPD: | Mkutano wa Kimataifa kuhusu Idadi ya watu na Maendeleo |
| MTCT: | Maambukizo kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto |
| MTP: | Mpango wa Muda wa Kati |
| NACP: | Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI |
| NGOs: | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| STIs: | Maambukizo Yanayoenezwa kwa Zinaa |
| STP: | Mpango wa Muda Mfupi |
| TACAIDS: | Tume ya Kudhibiti UKIMWI |
| UKIMWI: | Upungufu wa Kinga ya Mwili |
| VVU: | Virusi Vya UKIMWI |

## DIBAJI

UKIMWI ni janga la kitaifa na kimataifa, ambalo ili kudhibitiwa linahitaji hatua za pamoja katika ngazi ya taifa na kimataifa ambazo hatujawahi kuzichukua. UKIMWI ni tishio kubwa kwa uhai na maendeleo ya taifa letu. Tangu UKIMWI ulipogunduliwa nchini mwaka 1983, zaidi ya watu milioni mbili wameambukizwa virusi vya UKIMWI na maelfu wamepoteza maisha.

Asilimia 98 ya watu wazima sasa wanauelewa ugonjwa huu na jinsi unavyoambukizwa; lakini maambukizo ya virusi vya UKIMWI bado yanaendelea.

Jitihada za watafiti ndani ya nchi na duniani kote mpaka sasa bado hazijatupatia chanjo wala tiba ya UKIMWI. Dawa zilizopo, za kisasa na za jadi, zinasaidia kumpa mgonjwa ahueni tu na kumuongezea muda wa kuishi. Wakati huo huo, UKIMWI unaendelea kuua wazazi wetu, watoto wetu, ndugu zetu, rafiki zetu, wafanyakazi wenzetu, waajiri wetu na wafanyakazi wetu. UKIMWI husababisha mateso na maumivu makubwa kwa wagonjwa, usumbufu na gharama kubwa kwa familia, na hatimaye uchungu na ufukara katika familia. Hivyo, UKIMWI unaathiri sana maisha na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika taifa letu.

Athari za UKIMWI katika jamii yetu ni kubwa sana. Zaidi ya asilimia sabini ya wanaoambukizwa na kuugua UKIMWI ni watu wenye umri kati ya miaka 20 – 49 na hasa vijana. Kundi hilo ndilo linalotegemewa na familia na taifa kwa ujumla katika maisha, utendaji, uzalishaji mali, na hali ya baadaye ya taifa.

Hivyo, ni lazima tuupige vita UKIMWI kwa nguvu zetu zote. Lazima tuanze kwa kuzuia maambukizo ya virusi vya UKIMWI kwa wale karibu asilimia 85 ya watu wazima ambao hivi sasa hawana virusi vya UKIMWI, ili wabakie katika hali hiyo salama. Tuwahimize wakajipime kwa hiari yao, na kupata ushauri nasaha jinsi ya kuepuka kuambukizwa. Watakaojigundua wameambukizwa watapata msaada mapema wa ushauri nasaha, dawa za kudhibiti magonjwa yanayowaandama wenye virusi vya UKIMWI, na kuendelea kuishi maisha ya kawaida. Serikali kwa kushirikiana na wahisani, lazima tujenge uwezo wa kitaifa kutoa huduma hizi za kupima, kutoa ushauri nasaha, na kutibu magonjwa yanayowaandama wenye virusi vya UKIMWI

Vijana wetu wanahitaji msaada wa pekee wa kulindwa dhidi ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Lazima tuwaelimishe, tuwape ushauri nasaha na kuwawezesha mapema katika maisha yao kutumia njia bora za kuepuka maambukizo.

Katika kukabiliana na janga hili, kila mmoja wetu ana nafasi, hivyo kila mtu ajihusishe kikamilifu katika harakati za kudhibiti UKIMWI. Kila mmoja wetu atafakari mwenendo wake kimaisha, kuona kama mwenendo huo unamweka kiasi gani katika hatari ya maambukizo. Kila mtu ajiulize amefanya nini kuchangia vita hivi, na kama asingeweza kufanya zaidi.

Lazima tuvunje ukimya kuhusu UKIMWI. Lazima tuache miiko nayozuia majadiliano ya wazi katika familia, vijiji, jumuiya, na sehemu za kazi jinsi ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya JKIMWI. Lazima tujadili kwa uwazi na kwa makini mazingira ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni yanayochochea maambukizo, na namna ya kuzuia maambukizo yanayoletwa na zinaa. Pamoja na kuzuia maambukizo, lazima tujadili njia za kuwasaidia walioambukizwa na wanaoathirika na UKIMWI, wakiwemo mayatima katika jamii zetu. Kwa pamoja lazima tupige vita hali ya kuwabagua au kuwanyooshea vidole wenye virusi vya UKIMWI.

Sera hii ya taifa ni dira itakayotuongoza sote katika vita dhidi ya JKIMWI. Sera hii inaweka bayana masuala muhimu katika harakati za taifa za kudhibiti UKIMWI. Masuala haya ni pamoja na ushirikishwaji wa sekta zote katika vita dhidi ya UKIMWI, udhibiti wa maambukizo ya virusi vya UKIMWI, maadili na kanuni za kuzingatia katika upimaji wa virusi, haki na matunzo ya walioathirika na majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) katika kupambana na UKIMWI.

Hata hivyo kwa vile UKIMWI unagusa kila nyanja ya maisha ya amii yetu ya kila siku –kijamii, kitamaduni na kiuchumi –Sera hii tafanyiwa mapitio na kurekebishwa mara kwa mara kulingana na nabadiliko katika jamii na mwenendo wa mlipuko wa UKIMWI.

Sera hii ya Taifa ya UKIMWI, ambayo Serikali imeibuni kwa kushirikiana kwa karibu na washikadau na wahisani wetu, inawezesha kila sekta kuwa na mpango madhubuti wa utekelezaji katika kuzuia na kudhibiti kuenea kwa UKIMWI kwa makini sana. Viongozi katika kila sekta, na katika ngazi zote za uongozi, wajihusishe kikamilifu na kuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya UKIMWI. Lazima sote tutekeleze mipango na majukumu yanayotuhusu kwa makini sana.

Kwa pamoja tunaweza, na lazima tushinde. Uhai wetu kama taifa na kama watu unategemea sana ushindi huo.

Dar es Salaam,
26 Oktoba, 2001

BENJAMIN WILLIAM MKAPA,
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

# SURA YA 1

## .0. USULI

### 1.1. Athari ya VVU/UKIMWI

VVU/UKIMWI ni tatizo kubwa la maendeleo linaloathiri sekta zote. Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita mlipuko wa VVU/UKIMWI umeenea bila huruma na kuathiri watu katika nyanja zote za maisha na kuangamiza sehemu kubwa ya watu wanaoshiriki katika uzalishaji mali hususan wanawake na wanaume wenye umri kati ya miaka 20 na 49. Idadi inayoongezeka ya watu wanaokosekana katika maeneo yao ya kazi na vifo vinavyotokana na UKIMWI inaakisi udhihirisho wa awali wa janga hili linaloacha mateso na huzuni. Mengine yanahusu kupungua kwa matarajio ya muda wa kuishi, kuongezeka kwa uwiano wa watu tegemezi, kupungua kwa ongezeko la Pato Ghafi la Taifa, kushuka kwa tija, umaskini kuongezeka, kuongezeka kwa vifo vya watoto wachanga na watoto wadogo pamoja na ongezeko la idadi ya yatima. Watoto walio chini ya umri wa miaka kumi wanaathiriwa kwa kiwango kikubwa na athari za UKIMWI na kwao wao athari hizi zinadumu kwa muda mrefu kuliko kwa watu wazima. Janga hili ni tishio kubwa kwa maendeleo ya ustawi wa nchi kiuchumi na kijamii na lina athari kubwa na ya moja kwa moja kwa huduma za jamii na ustawi. Kutokana na kuenea kwa kiwango kikubwa kwa Virusi vya Ukimwi na kutokana na ukosefu wa tiba, athari za janga hili hazieleweki.

### 1.2. VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI na Umaskini

Imefahamika kwamba umaskini unasababisha sana kuenea na athari za VVU/UKIMWI. Kwa namna nyingine unazidisha madhara ya uambukizo wa VVU, kusababisha ufinyu wa kupata huduma za jamii na za afya. Umaskini unasababisha ufukara kwa kuwa unaleta kifo kwa sehemu muhimu ya watu wanaochangia katika uchumi wa jamii na ambao ndio wazalishaji wanaotegemewa hivyo kusababisha kupungua kwa kipato au uzalishaji. Kupotea kwa nguvu kazi kuna athari kubwa katika maendeleo kijamii na kiuchumi katika sekta zote na ngazi zote. Hatimaye gharama kubwa za matunzo na mazishi huacha

mzigo mzito kwa kaya, yatima na wategemezi ambao tayari wameelemewa, kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI (PLHAs) na uambukizwaji wa UKIMWI. Hivyo "kipengee cha umaskini" katika kaya kinapaswa kushughulikiwa sambamba na juhudi za Taifa za kupambana na UKIMWI.

## 1.3. Fedheha na VVU/UKIMWI

Fedheha zinazoambatana na Virusi vya UKIMWI ni moja ya changamoto muhimu katika kuzuia na kuudhibiti ugonjwa huu. Nchini Tanzania, kama ilivyo katika nchi nyingine kusini mwa Sahara, fedheha dhidi ya VVU/UKIMWI inabakia kuwa kubwa sana na inachangia sana katika kuchochea maambukizo ya VVU. Katika jamii yetu fedheha inayohusishwa na VVU/UKIMWI inaelekea kuhusishwa akilini mwa watu na tabia ya kujamiiana ambayo tena inachukuliwa kuwa ni tabia ya "uzinzi". Mtizamo huu unawaweka watu wanaoishi na VVU katika hali ya uhasama mkubwa na aibu, wanakabiliwa na hali ya kubaguliwa na wakati mwingine kutelekezwa. Kibaya zaidi ni kwamba fedheha hii inaambatana na usiri na kukanusha ambako kunazuia uwazi kuhusu VVU/UKIMWI na huzuia watu wasiombe ushauri na kupimwa VVU. Hali hii inawaacha mamia ya maelfu ya watu wanaoonekana kuwa wana afya ambao wameambukizwa VVU nao waambukize mamia ya maelfu ya watu ambao walikuwa hawajaambukizwa. Hivyo basi katika kupambana na ugonjwa huu, kila juhudi zitachukuliwa na sekta zote kwa viwango vyote katika kuvunja ukimya wa muda mrefu kuhusu VV/UKIMWI. Hizi zitawahusisha wataalamu wa afya, viongozi wa Chama na Serikali, viongozi wa dini, mashirika yasiyo ya kiserikali, watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, viongozi wa jumuiya na familia.

## 1.4. Ugharimiaji wa shughuli za Kitaifa za kukabiliana na VVU/UKIMWI

Serikali ina wajibu wa kusimamia na kuongoza masuala ya fedha katika shughuli za Taifa kuhusu uambukizo wa VVU/UKIMWI. Serikali imetenga Dola za Marekani milioni nane (8) kwa ajili ya shughuli za VVU/UKIMWI katika mwaka wa fedha 2001/2002 na Sekta na Halmashauri zote

zinatekeleza harakati za kupambana na VVU/UKIMWI Hata hivyo, kwa kuangalia gharama zilivyo kubwa Serikali pekee haina uwezo wa kutosha wa kugharimia programu za Kitaifa za kukabiliana na hali hiyo. Hivyo wabia wa kimaendeleo na Sekta binafsi nao wanawajibika kushiriki katika jukumu hili na kusaidia jitihada za Serikali. Kwa kuzingatia idadi kubwa sana ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wanaougua UKIMWI kuna umuhimu mkubwa wa jamii kujihusisha katika kuwasaidia yatima, na watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na matunzo ya nyumbani kwa wenye kuugua UKIMWI. Jamii itahitaji msaada wa fedha na wa kuungwa mkono kimawazo ili kumudu majukumu hayo. Hata hivyo, kwa kuzingatia hali mbaya ya uchumi kwenye halmashauri na jumuiya na hususan katika kaya, lazima zitafutwe mbinu za kupata fedha ili kuzisaidia jumuiya zinazojihusisha na kuwasaidia yatima na waathirika. Ni muhimu kubuni utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ili kusaidia jumuiya zinazojihusisha na shughuli za kusaidia walioathirika na VVU/UKIMWI na yatima kupitia halmashauri za mitaa. Mfuko huo unaweza kupata fedha kutoka halmashauri za mitaa, sekta binafsi, wabia wa kimaendeleo, mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs), mashirika ya ufadhili, vilabu na watu binafsi.

### 1.5. Msukumo wa Kisiasa na Kiserikali na Uongozi

VVU/UKIMWI ni tatizo la kimaendeleo ambalo matokeo *(impact)* yake yana madhara makubwa kijamii na kiuchumi. Udhibiti wake ni mgumu sana, na wenye gharama kubwa na unaohitaji kudhamiria na kujihusisha kwa vitendo. Uzoefu umeonyesha kwamba msukumo wa siasa na serikali ni muhimu katika kuongoza vita dhidi ya ugonjwa huu wa hatari. Inatarajiwa kwamba msukumo uliopo kisiasa na kiserikali utadumishwa katika ngazi zote. Ni muhimu kwamba uwajibikaji kisiasa na kiserikali katika vita dhidi ya ugonjwa huu hatari uimarishwe katika ngazi zote.

**1.6. Haja ya kuwepo na Sera ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI**

Katika kukabiliana na ugonjwa huu, Serikali kwa msaada wa kiufundi kutoka Programu ya Ulimwengu ya Shirika la Afya Duniani kuhusu UKIMWI (WHO-GPA) iliunda Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) chini ya Wizara ya Afya. Mpango huu ulianzisha Mpango wa Muda Mfupi (1985-1986) na Mipango mitatu ya muda wa kati ya miaka 5 (MTP); MTP-I (1987-1991) MTP-II (1992-1996) na MTP-III (1998-2002). Mwanzoni UKIMWI ulionekana kuwa ni tatizo la afya na kampeni za kulishughulikia zilihusisha Sekta ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI. Muitikio wa taifa katika kuushughulikia ugonjwa huu ulijumuisha kuweka mikakati ya kuzuia, kudhibiti na kupunguza athari ya UKIMWI kupitia elimu ya afya, kwa kushughulikia suala hili kimkoa, kushirikisha sekta mbalimbali na jumuiya. Hata hivyo muitikio huo haukuwa na matokeo ya kuridhisha kulingana na mfumuko wa ugonjwa kama ilivyokusudiwa. Juhudi za kitaifa zilikabiliwa na matatizo mbalimbali; ukosefu wa wafanyakazi na fedha, mfumo dhaifu katika uratibu na kutokuwepo na msukumo wa kutosha wa kisiasa na uongozi. Baadhi ya matatizo haya sasa yanashughulikiwa. Upo msukumo madhubuti wa siasa na uongozi kuanzia ngazi za juu zaidi. UKIMWI umetangazwa kuwa ni janga la Taifa na sasa ni mojawapo ya ajenda za maendeleo zinazopewa kipaumbele katika Serikali, ikiwemo kuondoa umaskini na uboreshaji wa huduma katika sekta ya jamii. Serikali imetenga Shillingi bilioni 7.2 ambazo ni karibu sawa na Dola za Marekani milioni 8 kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2001/2002 na sekta na halmashauri zote za mitaa zinatekeleza shughuli za kupambana na UKIMWI. Tume ya Kudhibiti UKIMWI imeanzishwa ili kuongoza na kuratibu muitikio wa sekta mbalimbali.

Utoaji wa madaraka mikoani umerahisisha ushirikishwaji wa watu katika utoaji wa maamuzi kwa masuala yanayoathiri maisha yao, ukiwemo UKIMWI. Kwa kuwa UKIMWI unaathiri sekta zote, udhibiti wake unahitaji uratibu mathubuti. Hivyo, ni muhimu kuwa na Sera ambayo itatoa mfumo, muelekeo na kanuni za jumla katika kuzuia kuenea, matunzo na msaada kwa wale

walioambukizwa na kuathirika na ugonjwa na kupunguza athari zake. Walakini, katika kuzingatia vipengele vizito vya UKIMWI kijamii, kimaadili, kisheria, kiutamaduni na kiuchumi. Sera itahitaji kupitiwa mara kwa mara ili kushughulikia masuala yatakayokuwa yakijitokeza.

### 1.7. Kanuni zinazolinda Sera ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI

(a) Changamoto mpya zinazojitokeza kutoka kwenye Mikutano ya Kimataifa k.v. Mkutano wa Kimataifa kuhusu idadi ya Watu na Maendeleo 1994 (ICPD), Mkutano wa Beijing wa 1995 na Mkutano wa Kijamii wa Dunia huko Copenhagen 1995, na mikataba yote ya haki za binadamu iliyotiwa saini na kuridhiwa na serikali vitaweka mfumo kwa ajili ya uundaji na utekelezaji wa SERA YA TAIFA YA KUDHIBITI UKIMWI.

(b) Wanajumuiya wote wana jukumu binafsi na la pamoja la kushiriki kwa ukamilifu katika kuzuia na kudhibiti uambukizo wa VVU/UKIMWI. Muitikio wa Taifa unapaswa kuhusisha Sekta mbalimbali na nyanja mbalimbali.

(c) Msukumo na uongozi madhubuti wa siasa na serikali katika ngazi zote ni muhimu katika kushiriki kwa ukamilifu kwenye vita dhidi ya VVU/UKIMWI.

(d) UKIMWI unazuilika! Kuenea kwa uambukizo kunazuilika kwa kubadilisha tabia binafsi, kwa hiyo elimu na taarifa kuhusu VVU/UKIMWI, mawasiliano kuhusu ubadilishaji wa tabia pamoja na mikakati ya kujikinga ni muhimu kwa ajili ya watu na jumuiya kuwa na ufahamu na ujasiri unaohitajika katika kuleta mabadiliko ya tabia ya jumuiya na mtu binafsi.

(e) Watu wana jukumu la kujilinda wao wenyewe na wengine wasiambukizwe kwa kujamiiana kusiko salama na/au kudungwa vitu ambavyo havijachemshwa au kufishwa vijidudu/kutakaswa.

(f) Jamii ina haki ya kupewa maelezo kuhusu namna ya kukinga watu wake dhidi ya maambukizo zaidi na

(g) Jumuiya na watu binafsi wana haki ya kukingwa kisheria kutokana na vitendo vya makusudi na kudhamiria vya kueneza VVU/UKIMWI huku haki za Watu wanaoishi na VVU au UKIMWI na watu wengine walioathirika zikilindwa kwa kutoa ushauri nasaha na msaada wa kijamii.

(h) Malengo ya muitiko wa taifa yatatekelezwa kwa ufanisi kwa mkabala wa jamii unaoeleweka ambao unajumuisha kuzuia maambukizo ya UKIMWI, matunzo na msaada kwa walioambukizwa na kuathiriwa na VVU na kwa ushirikiano wa karibu na watu wanaoishi na VVU au wenye UKIMWI.

(i) Fedheha zinazoambatana na UKIMWI huchangia kwa kiasi kikubwa kuchochea kuenea kwa maambukizo ya UKIMWI. Kupambana na fedheha hizi lazima kushirikishwe sekta na ngazi zote.

(j) Kuwepo na njia zinazokubalika na za gharama nafuu za uchunguzi na tiba ya maambukizo ya magonjwa ya zinaa na maambukizo mengine yanayoambatana na hayo katika huduma zote za afya.

(k) Ushauri wa kabla na baada ya kupima VVU uzingatie maadili ya kitaaluma, mkazo ukiwa katika utunzaji siri na kutoa taarifa kwa ridhaa ya mhusika.

(l) Watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI wana haki ya kupata matunzo mazuri ya afya na huduma nyingine za jamii, ikiwa ni pamoja na kinga ya kisheria dhidi ya aina zote za ubaguzi na kutokuzingatia haki za binadamu. Hata hivyo, watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI wanaweza kutakiwa kugharimia baadhi ya Tiba ya Hali ya juu ya Kusogeza mbele Siku za Kuishi (HAART).

(m) Utafiti ni sehemu muhimu sana katika kukabiliana na VVU/UKIMWI, ukijumuisha kinga na kudhibiti. Tafiti za sekta na nyanja mbalimbali zitakazofanywa zitafuata kanuni za utafiti za sekta na idara husika.

(n) Kwa kuwa UKIMWI ni tatizo la kijamii, kiutamaduni na kiuchumi, wanawake na watoto wanahitaji uangalifu wa ziada wa kuwakinga na madhara ya maambukizo yanayoongezeka ya UKIMWI katika mazingira mbalimbali ya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi kama ilivyoelezwa katika Sera ya Taifa ya Jinsia na Usawa.

(o) Kwa kuwa makundi yaliyo katika hatari kubwa yanachangia sana katika kueneza UKIMWI, mikakati inayofaa ya kupunguza madhara ya maambukizo ya UKIMWI miongoni mwa makundi mahsusi yaliyo katika hatari kubwa ya kuambukizwa haina budi kuwekwa.

(p) Kwa kuangalia mzunguko unaojirudia kati ya VVU/ UKIMWI na Umaskini, kukabiliana na udhibiti wa ugonjwa huu unaoambukiza kunapaswa kufanywe sambamba na jitihada za kuondoa umaskini.

# SURA YA 2

## 2.0. HALI ILIVYO KUHUSU UKIMWI

### 2.1. Hali halisi ilivyo sasa

Mpaka kufikia mwisho wa mwaka 1999 inakisiwa kuwa watu wazima na watoto milioni 33.6 walikuwa wakiishi na VVU na milioni 16.3 walikuwa tayari wamefariki dunia. Mwaka huohuo kulikuwa na maambukizo mapya ya watu milioni 5.6 ambao kati yao milioni 4 walikuwa Afrika Kusini mwa Sahara. Kwa ujumla, inakisiwa kuwa watoto milioni 13.2 wamekuwa yatima ulimwenguni kutokana na VVU/ UKIMWI na karibu milioni 9.4 wamo Afrika peke yake.

Katika bara la Afrika taarifa za wagonjwa wa kwanza wa UKIMWI zilitolewa mapema miaka ya 1980. Mpaka 1987 ugonjwa ulikuwa umekwishaenea katika karibu nchi nyingi za Afrika Kusini mwa Sahara. Kati ya wagonjwa milioni 33.6 wa UKIMWI duniani karibu wagonjwa milioni 23 wanatoka Afrika Kusini mwa Sahara, Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi zilizoathirika sana.

Nchini Tanzania wagonjwa watatu wa kwanza wa UKIMWI waliripotiwa mwaka 1983 huko Mkoa wa Kagera. Hadi Mwaka 1986 mikoa yote ya Tanzania Bara ilikuwa imekwishakuwa na wagonjwa wa UKIMWI. Mpaka kufikia mwishoni mwa 1999 kulikuwa na wagonjwa 600,000 wa VVU/UKIMWI na idadi kama hiyo ya yatima. Inakadiriwa pia kwamba zaidi ya watu milioni 2 wameambukizwa Virusi vya Ukimwi; asilimia 70.5 wakiwa katika umri wa miaka 25-49, na asilimia 15 miaka 15-24. Zaidi ya watoto wachanga waliozaliwa 72,000 walikuwa wameambukizwa virusi vya UKIMWI . Wanawake wanapata maambukizo katika umri mdogo. Kati ya maambukizo mapya kwa wanawake asilimia 69 walikuwa na umri wa miaka 15-24.

### 2.2. Jinsi UKIMWI unavyoenezwa

UKIMWI unaenezwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine hasa kwa tendo la kujamiiana na mtu wa jinsia

tofauti ambapo ni kiasi cha asilimia 90 ya maambukizo yote. Uambukizo wa UKIMWI unaweza pia kuenezwa kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wake wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua au kutokana na kunyonyesha. Njia nyingine za kuambukiza UKIMWI zinaweza kuwa kupitia damu yenye virusi, bidhaa za damu, viungo vya mwili vya kuwekewa au vipandikizi vya mifupa na tishu.

### 2.3. Hatari ya Maambukizo ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI

Kutokana na ukweli kwamba maambukizo ya UKIMWI hutokana zaidi na njia ya kujamiiana na mtu wa jinsia tofauti, VVU/UKIMWI ni tatizo la kijamii, kiutamaduni na kiuchumi, ambalo linagusa mitindo binafsi ya maisha ya watu. Hivyo hatari ya uambukizo wa UKIMWI ni kubwa sana miongoni mwa vijana, na hususan wasichana. Wasichana na wanawake katika mazingira yetu kijamii na kiutamaduni wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa UKIMWI kwa kuwa hawana udhibiti wa ujinsia wao. Umaskini unaongeza hatari ya kuambukizwa UKIMWI kwa kuwa baadhi ya wanawake hujihusisha na tabia ya hatari kubwa ya kujamiiana kwa ajili ya kujikimu.

## SURA YA 3

## 3.0. MALENGO MAKUU YA SERA YA TAIFA YA KUDHIBITI UKIMWI

### 3.1. Utangulizi

Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ni kuweka mfumo wa uongozi na uratibu wa Sekta mbalimbali katika kukabiliana Kitaifa na Virusi vya UKIMWI/UKIMWI. Sera hii inawajibisha kila sekta kuandaa na kutekeleza mipango ifaayo ya kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa, kukinga na kusaidia makundi yaliyoathirika na kupunguza athari za kijamii na kiuchumi za VVU/UKIMWI. Inaweka pia mfumo wa kuimarisha uwezo wa taasisi, jumuiya mbalimbali na watu binafsi katika sekta zote kuzuia kuenea kwa mlipuko wa UKIMWI. Kwa kuwa ni tatizo la kijamii, kiutamaduni na

kiuchumi, kuzuia na kudhibiti VVU/UKIMWI kutategemea sana kushiriki kwa ukamilifu kwa jumuiya katika kuzuia, matunzo na kutoa msaada. Halmashauri za serikali za mitaa zitakuwa mahali pa kuanzia kuzishirikisha na kuziratibu sekta za umma na binafisi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na vikundi vya kidini katika kupanga na kutekeleza shughuli za kukabiliana na ugonjwa huo hususan katika kushirikisha jamii. Halmashauri za serikali za mitaa zitafaidika na uzoefu mzuri zaidi katika mikabala ya jumuiya katika baadhi ya halmashauri hapa nchini.

## 3.2. Madhumuni mahususi ya Sera

### (a) Kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI

(i) Kuanzisha na kuongeza mwamko wa kutambua UKIMWI kwa Kampeni maalumu, taarifa, elimu, na mawasiliano ya kubadilisha tabia katika ngazi zote kwa sekta zote. Hivi vinasaidia kuhusisha jumuiya na kuipa uwezo wa kuanzisha mikabala inayofaa katika kuzuia maambukizo ya UKIMWI, matunzo na msaada kwa wale walioambukizwa na kuathiriwa na ugonjwa wakiwemo wajane na yatima.

(ii) Kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI kwa:

aa. Kuhakikisha usalama wa damu na bidhaa za damu wanazopewa wagonjwa.

bb. Kuhimiza tabia nzuri za kujamiiana kwa usalama zaidi kwa kuwa na wenza waaminifu, kutokufanya mapenzi ya kuingiliana na kutumia kondomu kwa mujibu wa uamuzi wa watu wenye uelewa wa kutosha. Suala la msingi katika kubadili njia za kuzuia maambukizi kutategemea vipimo.

cc. Kuwahi kutibu ipasavyo maambukizo ya magonjwa ya zinaa (STIs) katika vituo vya afya, mkazo mkubwa ukiwa katika makundi yaliyo katika hatari kubwa na kufanya uchunguzi mapema wa maambukizo ya UKIMWI kwa kupatiwa ushauri na vipimo vya hiari.

**(b) Kupima Virusi vya UKIMWI**

(i) Kuhimiza uchunguzi wa mapema wa maambukizo ya UKIMWI kwa vipimo vya hiari na ushauri nasaha wa kabla na baada ya kupimwa. Lengo kuu ni kuithibitishia na kuitia moyo asilimia 85-90 ya watu ambao hawana UKIMWI kuchukua hatua za kufaa za kutokuambukizwa na wale wenye VVU kupewa msaada unaofaa na ushauri nasaha na matunzo ya kukabiliana na hali zao, kusogeza mbele siku za kuishi na kutokuwaambukiza wengine.

(ii) Kupanga mipango ya mafunzo ya ushauri nasaha na kutambuliwa rasmi kwa programu za mafunzo nchini Tanzania ili kuhakikisha kwamba ushauri nasaha kuhusu VVU/UKIMWI unafuata kanuni za kawaida za utendaji.

**(c) Huduma kwa watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI**

(i) Kutoa huduma za ushauri nasaha na msaada wa kijamii kwa watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI pamoja na familia zao.

(ii) Kupiga vita fedheha na kuendelea kuishi kwa matumaini.

(iii) Kutoa matunzo na tiba ya kufaa kwa kuboresha mfumo wa utunzaji afya wenye lengo la kuhimiza hali bora ya maisha.

(iv) Kuanzisha mfumo wa rufaa na ruhusa utakaounganisha huduma za hospitali na huduma za jumuiya kwa uhusiano wa kukamilishana wa kudumu huku ikihakikishwa kwamba ubora wa usimamizi wa matunzo hospitalini unalingana na ule wa matunzo ya nyumbani.

(v) Kuhakikisha kupatikana kwa dawa muhimu za kutibu maambukizo yanayoambatana na ugonjwa. Kwa hali ilivyo sasa upatikanaji wa dawa yenye uwezo mkubwa wa kusogeza mbele siku za kuishi (HAARD) katika soko, watu wanaoishi na VVU na

wenye UKIMWI watatakiwa kulipia gharama za dawa hizo. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itatafuta mbinu za ununuzi na usimamizi wa HAARD.

(vi) Kuhakikisha kuwa gharama za ushauri nasaha na matunzo ya nyumbani zinaonyeshwa katika Bajeti za Serikali kuu na Halmashauri za mitaa za Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii. Mbinu zitatafutwa za kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ili kusaidia juhudi za jumuiya zikiwemo matunzo ya nyumbani na ya yatima.

(vii) Kuzishirikisha na kuzisaidia jumuiya katika kutoa huduma za matunzo za jumuiya na nyumbani

**(d) Dhima na Ugharimiaji Kisekta**

(i) Kuimarisha dhima ya sekta zote za umma, binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) vikundi vya kidini, watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI, Mashirika ya Kijumuiya (CBOs) na makundi mengine mahususi kuhakikisha kuwa washika dau wote wanahusika kikamilifu katika shughuli zinazohusu VVU /UKIMWI na kuweka mfumo wa uratibu na ushirikiano.

(ii) Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na msukumo madhubuti kisiasa na kiserikali, uongozi na uwajibikaji katika ngazi zote.

(iii) Kuweka mfumo wa uratibu wa shughuli za kuchangisha fedha, upangaji bajeti, na utafutaji wa watumishi na vifaa kwa ajili ya shughuli zinazohusika na VVU/UKIMWI katika Tanzania nzima.

(iv) Kuhimiza sera za kisekta ili kukabiliana na VVU/ UKIMWI.

(v) Kuhimiza na kukuza moyo wa kushiriki katika shughuli kijumuiya zinazohusu masuala ya UKIMWI. Hizi ni pamoja na uwakilishi wa kijumuiya katika mpango wa Kitaifa na kiwilaya wa kuchangisha fedha, upangaji mikakati na utekelezaji vitakavyofanywa na sekta zote. Hujumuisha pia upangaji wa mikakati katika ngazi za kata na vijiji kwa ajili ya uzuiaji wa kuenea kwa VVU na maambukizo ya magonjwa ya zinaa pamoja na matunzo na kuwasaidia wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI, wategemezi, familia zao na yatima.

**(e) Utafiti**

((i) Kushiriki katika utafiti kuhusu VVU/UKIMWI, Kitaifa na Kimataifa na kuanzisha mfumo wa kusambaza taarifa za kisayansi zinazotokana na utafiti huu huku maadili yanayotawala kanuni za kushughulikia masuala ya VVU/UKIMWI yakizingatiwa.

(ii) Serikali itafuatilia kwa karibu na kushiriki katika jitihada za kutafuta chanjo ya UKIMWI.

**(f) Masuala ya utungaji Sheria na Sheria**

Kuanzisha mfumo wa kisheria kwa kutunga sheria kuhusu UKIMWI kwa kuzihusisha sekta mbalimbali katika kudhibiti VVU/UKIMWI na kuyashughulikia kisheria na kimaadili na kuangalia upya kisheria hali ya familia zilizoathiriwa na VVU/UKIMWI ili kuwawezesha kupata mali ya familia mara baada ya kifo cha mzazi/ wazazi wao.

**(g) Madhumuni mengine**

(i) Kufuatilia jitihada za kuhamasisha jumuiya kwa kuishi kwa matumaini na VVU/UKIMWI ili kukabiliana na athari za ugonjwa huku haki za wale walioambukizwa na kuathirika moja kwa moja na VVU/UKIMWI zikilindwa katika jamii.

(ii) Kuainisha ukiukaji wa haki za binadamu kwa VVU/ UKIMWI na kuwakinga watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI dhidi ya aina zote za ubaguzi na ukosefu wa haki katika jamii.

(iii) Kutoa matibabu yanayofaa kwa maambukizo yanayoambatana na ugonjwa katika ngazi zote za mfumo wa huduma za afya.

(iv) Kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na Vikundi vya Dini katika vita dhidi ya matumizi mabaya ya madawa ya kulevya ambayo yanaongeza hatari ya kuenea kwa UKIMWI.

(v) Kupiga marufuku matangazo yanayopotosha kuhusu madawa na vitu vingine vinavyozuia, kutibu na matunzo kwa waathirika wa VVU/UKIMWI.

## SURA YA 4

## .0. HAKI ZA WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI/ UKIMWI

### 4.1. Madhumuni

Madhumuni makuu ni kulinda haki za watu wanaoishi na VVU/UKIMWI ili kuinua ubora wa maisha yao na kupunguza fedheha. Kwa ajili hiyo Tanzania itashirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Kimataifa na Umoja wa Mataifa kupitia upya na kuirekebisha miongozo inayohusu Haki za Binadamu na VVU/UKIMWI.

(a) Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI wanastahili kupata mahitaji yote ya msingi na haki zote za raia, za kisheria na za binadamu bila ubaguzi wowote kijinsia au hali.

(b) Watu wanaotafuta taarifa au ushauri nasaha, matibabu na matunzo ya VVU/UKIMWI wanastahili kupewa haki sawa na mtu mwingine yeyote anayehitaji huduma nyingine za afya/jamii.

(c) Kuambukizwa UKIMWI hakutakuwa msingi wa kubaguliwa katika elimu, ajira, afya na huduma nyingine yoyote ya kijamii. Upimwaji wa VVU kabla ya kupatiwa ajira hautahitajika. Watu ambao tayari wameajiriwa hawatahitajika kupima VVU moja kwa moja au kwa namna fulani. Maambukizo pekee ya VVU hayamaanishi kwamba mtu hafai kufanya kazi au kuwa msingi wa kufukuzwa kazi. Watu wenye VVU/UKIMWI watastahili kupata mafao kutoka ustawi wa jamii sawa na wagonjwa wengine miongoni mwa wafanyakazi.

(d) Taarifa na elimu kuhusu VVU/UKIMWI yanayolenga tabia na mwenendo wa waajiriwa na waajiri pamoja vitakuwa ni sehemu ya harakati za kukabiliana na UKIMWI mahali pa kazi.

(e) Hatua za kukinga umma kutokana na kuenea kwa VVU/ UKIMWI mahali pa kazi zitachukuliwa na mashirika yanayohusika.

(f) Vijana wa umri wa kubalehe wana haki sawa ya kutunziwa siri na faragha pamoja na kuombwa ridhaa ya kufahamishwa, ili washiriki katika ushauri nasaha.

(g) Umma una haki ya kuwajibika kwa upande wa watu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI kuhusiana na kinga ya VVU/UKIMWI.

(h) Wafungwa wana haki ya kupewa taarifa za msingi kuhusu UKIMWI, kupata ushauri nasaha na vipimo vya hiari, na matunzo, yakiwemo matibabu ya maambukizo ya magonjwa ya zinaa.

(i) Kuhakikisha kuwa masuala ya Haki za Binadamu kuhusu UKIMWI yanafuatwa, yakiwemo:

aa. Haki za kutokubaliwa, ulinzi sawa na usawa mbele ya Sheria;

bb. Haki ya kutafuta na kunufaika na hifadhi;

cc. Haki ya kuwa huru na salama;

dd. Haki ya kufikia viwango vya hali ya juu kimwili na kiakili;

ee. Haki ya kuwa na faragha;

ff. Haki ya kuwa na uhuru wa kujiunga na vyama;

gg. Haki ya uhuru wa kutoa mawazo na kusema na haki ya kupokea na kutoa taarifa bila ya kubughudhiwa;

hh. Haki ya kuoa/kuolewa na kuwa na familia;

ii. Haki ya kufanya kazi;

jj. Haki sawa ya kupata elimu;

kk. Haki ya kuishi maisha mazuri;

ll. Haki ya kulindwa, kupata msaada na ustawi katika jamii;

mm. Haki ya kuchangia maendeleo ya kisayansi na manufaa yake;

nn. Haki dhidi ya mateso na ukatili, vitendo visivyo vya kibinadamu au kudhalilishwa au adhabu.

# 5. KUZUIA KUENEA KWA UKIMWI UNAOTOKANA NA KUJAMIIANA

## 5.1. Madhumuni

Maambukizo ya UKIMWI yanazuilika. Kwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya maambukizo yote hutokana na kujamiiana, kuzuia kuenea kwa magonjwa yanayotokana na kujamiiana ni msingi wa udhibiti wa VVU/UKIMWI. Hivyo lengo kuu ni kuelimisha umma kuhusu hatari na mabadiliko ya tabia ambavyo vinamuweka mtu katika hatari ya kuambukizwa au kueneza UKIMWI na magonjwa mengine yanayoambukizwa kwa zinaa ili kupunguza kuenea kwa ugonjwa. Kuenea kwa UKIMWI kunaongezeka kwa kiwango kikubwa kwa wale ambao wana wapenzi wengi na ambao wanajamiiana bila kujikinga. Sekta zote zitashirikishwa katika kuhimiza elimu kwa umma katika ngazi zote na hususan katika ngazi ya jumuiya na kuipa jumuiya uwezo wa kuanzisha mikabala inayofaa katika kuzuia kuenea kwa UKIMWI. Haya yanajumuisha kuwa mwaminifu kwa huyo mpenzi, kujizuia kufanya kitendo hicho, kutumia kondomu kwa usahihi na uthabiti, kupewa ushauri na kupimwa kwa hiari, kutokukimbilia kujihusisha mapema na vitendo vya kujamiiana kulingana na uamuzi binafsi wa mtu.

## 5.2. Kwa Vijana Walioko Shuleni na Kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu

Sekta ya elimu ni miongoni mwa sekta ambazo zimeathiriwa sana na VVU/UKIMWI. Ugonjwa huu umesababisha kushuka kwa ubora wa elimu kwa kuwa huua walimu na wanafunzi wengi. Mwelekeo wa kuongezeka kwa VVU/UKIMWI kutokana na kutokuacha tabia hiyo na vifo vya walimu na wanaoacha shule ni tishio kubwa sana kwa maendeleo ya elimu. Watoto wa shule, vijana katika umri wa kubalehe na watu wazima vijana ndio wanaoathiriwa sana na maambukizo ya UKIMWI. Wizara inayohusika na masuala ya elimu na idara nyingine za umma na serikali za elimu ya juu kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) itaweka mikakati inayofaa katika kuzidisha uenezaji

wa elimu ya UKIMWI shuleni, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa zisizochujwa kuhusu UKIMWI katika shule za msingi na sekondari. Utoaji wa taarifa zinazohusu UKIMWI unapaswa kuanzishwa mapema kadiri iwezekanavyo ili kuwaepusha watoto ambao bado hawajajihusisha na masuala ya kujamiiana kabla hawajajiingiiza katika vitendo vya kujamiiana ili kuwapa vijana maarifa na ujuzi wa kutosha wa kujikinga wao wenyewe na wenzao dhidi ya kuenea kwa UKIMWI. Elimu ya afya ya uzazi na jinsia inapaswa kuingizwa kwenye mtaala wa Shule.

### 5.3. Vijana walio nje ya Shule

Wizara inayohusika na masuala ya maendeleo ya vijana, kwa kushirikiana na Halmashauri za Serikali za Mitaa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na vikundi vya dini itaanzisha programu shirikishi za elimu ya jinsia na afya ya uzazi kuhusu UKIMWI kwa vijana walio nje ya shule. Vijana wanapaswa kupewa taarifa sahihi ikiwa ni pamoja na mikakati ya kuzuia ikiwemo kuendeleza matumizi sahihi na thabiti ya kondomu, kuacha kitendo hicho na uaminifu, na kujitolea kupewa ushauri nasaha na kupimwa kwa hiari. Wasichana pia washauriwe wajiepushe na mimba zisizopangwa. Baada ya kuwezeshwa kupewa taarifa vijana wanapaswa kutiwa moyo na kusaidiwa kupanga mikakati yao wenyewe.

### 5.4. Kwa Watu Wazima

Serikali, Halmashauri za Serikali za Mtaa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), Mashirika ya Jumuiya (CBOs) na vikundi vya dini vitaanzisha Programu za Taarifa, Elimu na Mawasiliano (IEC) kuhimiza njia za kujamiiana zilizo salama ikiwa ni pamoja na uaminifu, kuacha, na matumizi sahihi na thabiti ya kondomu kulingana na uamuzi wa mtu binafsi.

### 5.5. Kwa watu wenye wapenzi zaidi ya mmoja na wanaofanya Biashara ya Ngono

Programu za Taarifa, Elimu na Mawasiliano (IEC) na ushauri nasaha zitaenezwa na kukubalika kwa watu wenye wapenzi zaidi ya mmoja wakiwemo wanaofanya biashara ya ngono ili waweze kufuata njia salama za kujamiiana.

**wa watumiaji wa Dawa za Kulevya**

ıshirika ya Serikali yanayoshughulikia matumizi mabaya dawa kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI ACAIDS) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na vikundi a dini vitaimarisha shughuli zao za kinga na kutekeleza ıduma zinazolengwa za Taarifa, Elimu na Mawasiliano ushauri kwa watumiaji dawa za kulevya.

**wa Watu Wanaoishi na VVU/UKIMWI**

atu wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI watahimizwa ıfuata kanuni za afya ambazo zitawawezesha kuishi kwa atumaini na virusi hivyo. Nyenzo na huduma zitapatikana kuwarahisishia ubadilishaji wa tabia kiafya.

**yombo vya Habari**

ndelezaji wa elimu kwa umma na uhamasishaji ni muhimu tika kuudhibiti ugonjwa. Kwa hiyo dhima ya vyombo vya ıbari ni muhimu sana. Vyombo vya habari vinavyoandika ıhusu habari za mila na desturi kwa kushirikiana na ashirika mengine yanayohusika vitakuwa mstari wa mbele tika kuuelimisha umma kuhusu VVU/UKIMWI. Vyombo a habari vinapaswa kuhusishwa kwa ukamilifu katika ıchunguza changamoto za vitendo katika udhibiti wa IMWI na mwitiko wa sekta mbalimbali katika jamii, ikiwa pamoja na sekta binafsi. Machapisho ya kisayansi kuhusu ielekeo ya uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko na shughuli utafiti kuendeleza njia zilizo salama yatasambazwa katika ajarida ya kitaaluma na kupitia vyombo vya habari.

**ushiriki kwa Jamii**

ımii ndio kiini cha kudhibiti UKIMWI. Jamii ielimishwe kwa kamilifu kuhusu VVU/UKIMWI na changamoto halisi za aisha katika kujikinga na matunzo yake. Jumuiya zihimizwe ı zisaidiwe kuanzisha mikabala inayofaa kupunguza aambukizo ya UKIMWI na matunzo kwa Watu Wanaoishi ı VVU na wenye UKIMWI (PLHAs) na yatima katika maeneo o. Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) itahimiza sekta te, Halmashauri za Serikali za Mitaa, vikundi vya dini, ashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na Mashirika ya ımuiya (CBOs) kuhamasisha jumuiya kupanga na ıtekeleza shughuli za udhibiti wa UKIMWI katika jumuiya zao.

### 5.10. Kondomu

Upo ushahidi mkubwa sana kuhusu umadhubuti na kufaa kwa kondomu iwapo zitatumiwa kwa usahihi na kwa uthabiti katika kuzuia maambukizo ya UKIMWI. Kondomu zenye ubora wa kufaa zitatafutwa na kuzifanya zipatikane na tena kwa bei nafuu. Sekta binafsi itahimizwa kutafuta na kuuza Kondomu zenye ubora unaofaa ili ziweze kupatikana kwa urahisi katika maeneo ya mijini na vijijini.

### 5.11. Kukinga na Kusimamia Maambukizo ya Magonjwa ya Zinaa (STIs)

Maambukizo ya magonjwa ya zinaa yatatakiwa kufanyiwa uchunguzi mapema, kutibiwa, kukingwa na kudhibitiwa kwa sababu yana uwezo mkubwa wa kusaidia kuenea kwa VVU/UKIMWI. Haya yatajumuisha kumtaarifu mpenzi, kutoa ushauri nasaha, na kuthibitisha usimamiaji wa dalili zinazoweza kuambatana na maambukizo ya magonjwa ya zinaa mara kwa mara.

(a) Uelimishaji na utoaji taarifa kuhusu maambukizo ya magonjwa ya zinaa vitazidishwa ili watu wachukue hatua ya kujiepusha na maambukizo ya magonjwa ya zinaa na kutafuta tiba mapema.

(b) Watoa huduma za afya wa kada zote watapatiwa mafunzo ili kupata maarifa na ujuzi muhimu katika kuzuia, kufanyiwa uchunguzi mapema na kusimamia masuala yanayoambatana na maambukizo ya magonjwa ya zinaa.

(c) Kutoa ushauri nasaha na kumtaarifu mwenza/mpenzi kutakuwa ni sehemu ya matunzo kulingana na miongozo ya usimamizi wa maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

(d) Serikali itasimamia upatikanaji wa huduma kwa ajili ya maambukizo ya magonjwa ya zinaa na kuhakikisha kwamba pale ambapo matibabu kwa maambukizo ya magonjwa ya zinaa si bure, yatapatikana kwa gharama nafuu kulingana na sera iliyopo ya kuchangia gharama.

**Uambukizaji kwa njia ya damu na bidhaa za damu viungo vya mwili na majimaji ya mwili**

Tafiti zilizofanywa nchini Tanzania zimeonyesha kuwepo kwa kiwango kikubwa cha maambukizo ya UKIMWI katika damu na bidhaa za damu ambavyo watu wanajitolea kutoa. Data zinaonyesha kwamba, mmoja kati ya watu kumi wanaojitolea damu anaweza kueneza VVU kupitia damu au bidhaa za damu alizotoa. Aidha VVU/UKIMWI, magonjwa mengine kama homa ya manjano *(Hepatitis B na C)*, kaswende na maambukizo mengine ya magonjwa ya zinaa yanaweza kuenezwa kwa damu au bidhaa za damu.

Serikali imeweka miongozo ya kupunguza kuenea kwa UKIMWI kutokana na utoaji wa damu. Vituo vyote vinavyokusanya damu havina budi kufuata miongozo ifuatayo:-

(a) Serikali itaimarisha huduma ya kitaifa ya utoaji damu kwa kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya vinatoa damu iliyopimwa na salama.

(b) Vituo vya uchunguzi vilivyoidhinishwa vitatoa huduma za ushauri nasaha kabla na baada ya kupima watu wote wanaojitolea kutoa damu.

(c) Utoaji wa damu isiyofanyiwa uchunguzi na madaktari utakuwa ni kosa linalostahili adhabu.

(d) Vituo vinavyotoa huduma za masuala ya ugumba, upandikizaji viungo na tishu nyingine za mwili vitahakikisha kuwa viungo hivyo hai vinachukuliwa kwa watu wasio na UKIMWI.

(e) Jumuiya zitaelimishwa ili zitambue kwamba kupewa damu kutakuwa ni uamuzi wa mwisho katika tiba, na kama ikiwezekana damu ya "autologous" itatumika. Tiba ya mapema ya magonjwa ya kuambukiza na lishe bora vitahimizwa ili kuwaepusha kina mama na watoto wengi na hatari inayotokana na kuwekewa damu.

## 5.13. Uambukizaji kwa tiba ya upasuaji, kutoga, na tiba ya meno.

Kuna hatari ya kuenea kwa UKIMWI kwa kutumia vifaa vya operesheni, meno na vya kuchanja mwili. Vifaa na vyombo vya kutibia meno visivyomunizwa (sterilization) vina madhara makubwa, ambayo yanaweza kupunguzwa kwa umunizaji unaofaa.

(a) Utumiaji wa Vifaa vinavyotumiwa mara moja tu na kuumia kwa bahati mbaya

(i) Ili kupunguza hatari ya kuambukizwa, vifaa vya kutumiwa mara moja tu vikiwa ni pamoja na sindano na mabomba ya sindano vitatumiwa katika vituo vyote vya afya. Ikitokea kwamba vifaa vya kudungia vya kutumiwa mara moja tu havipatikani, vifaa vilivyotumika vitatumiwa baada ya kumunizwa.

(ii) Serikali itahakikisha kuwa watoaji wa huduma za afya wanapatiwa mafunzo ya kutosha kuhusu taratibu za umunizaji na umuhimu wake.

(iii) Serikali itasimamia na kufanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa taratibu zinafuatwa kwa ushirikiano wa watoaji wa huduma hospitalini, nyumbani na kwenye saluni za urembo.

(iv) Serikali itaendeleza kampeni dhidi ya ukeketaji na jumuiya iliyoko katika sehemu husika.

(v) Serikali itaandaa miongozo itakayofafanua kwa uwazi hatua za kuchukuliwa wakati mfanyakazi anayetoa huduma za afya anapoumia kwa bahati mbaya na/au anapokuwa katika hatari ya kuambukizwa VVU kwa kutumia mkabala wa dharura wa Shirika la Afya Duniani baada ya mtu kuambukizwa (PEP).

(vi) Chombo cha kutoa fidia na bima ya matibabu kwa wafanyakazi wanaotoa huduma za afya ambao wanathibitika kuwa hawakuwa na VVU kitaanzishwa ili kushughulikia watu watakaoambukizwa kwa bahati mbaya wakati wa kutekeleza majukumu yao.

(vii) Masaibu ya wagonjwa ambao wanaweza kuwa wameambukizwa VVU kwa bahati mbaya wakati wanapokuwa wanatibiwa yatashughulikiwa sawa na yale ya watoa huduma.

(viii) Miongozo kuhusu usimamizi, ushughulikiaji wagonjwa wenye magonjwa ya kuambukiza na utupaji wa vifaa vyenye maambukizo itafuatwa.

b) Uelimishaji wa watu wanaotumia huduma za afya

(i) Elimu ya umma itatolewa ili kuhakikisha kuwa watumiaji wa huduma za afya, matunzo nyumbani wanajua na kuomba vifaa vya kudungia vilivyomunizwa ikiwa ni pamoja na vifaa kama glavu. Umma utaelezwa kuhusu muundo wa mfumo wa utoaji taarifa kwa ajili ya kuripoti malalamiko na maoni ya uboreshaji wa mfumo.

(ii) Ikitokea kwamba uenezaji wa VVU na maambukizo ya magonjwa ya zinaa au magonjwa mengine kwa wagonjwa na wateja wa huduma nyingine zinatokana na uzembe wa watoaji huduma, mgonjwa au mteja atachukua hatua kulingana na sheria zilizopo.

**Kuzuia uambukizaji wa UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto (PMTCT)**

Uambukizaji kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto mpaka sasa ni chanzo cha kawaida cha maambukizo ya VVU kwa watoto. Uwezekano wa kuishi kwa watoto wanaopata maambukizo ya VVU kutoka kwa mama ni mdogo. Karibu asilimia 25-35 ya wanawake wote wenye UKIMWI wataambukiza watoto wao wachanga. Pia kuna uwezekano wa asilimia 15-20 wa watoto kuambukizwa wakati wa kunyonya maziwa ya mama. Ushauri nasaha na upimaji wa mama wajawazito kwa hiari yao, na kama ikiwezekana, waume au wapenzi wao utahimizwa katika ngazi zote.

**(a) Maambukizo ya Kabla ya Kuzaa**

(i) Elimu kuhusu hatari ya maambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto itatolewa kwa wanawake wote wenye umri wa kuzaa na wapenzi/wenza wao.

(ii) Utoaji ushauri nasaha na uzuiaji mimba kwa kina mama na wapenzi/wenza wao wenye VVU.

(iii) Taarifa na elimu ya uchaguzi wa teknolojia mbadala ikiwa ni pamoja na matibabu ya kufunga vizazi kwa wanawake wajawazito walioambukizwa.

**(b) Uambukizaji wakati wa kujifungua**

Wataalamu wa afya wanatumia mbinu za kisasa, matibabu na njia za kusimamia ujauzito na kujifungua. Watachagua njia za kupunguza hatari ya kumuambukiza mtoto UKIMWI.

**(c) Uambukizaji baada ya Kujifungua**

Ili kuzuia uambukizaji wa UKIMWI kupitia unyonyeshaji wa maziwa ya mama, huduma zifuatazo zinapaswa kutolewa: -

(i) Ushauri nasaha binafsi kuhusu unyonyeshaji wa maziwa ya mama.

(ii) Ushauri nasaha kwa waume, wapenzi na ndugu wengine kuhusu unyonyeshaji wa maziwa ya mama na maambukizo ya UKIMWI, na kutoa msaada wa hali na mali kumsaidia mama na/au familia.

(iii) Kuuelimisha umma kuhusu mahitaji ya msaada kwa mama mwenye UKIMWI kwa matunzo yake mwenyewe na uzuiaji wa uambukizo kwa mtoto.

(iv) Ushauri nasaha kuhusu vyakula mbadala vyenye afya kwa mtoto au mambo ya kufanya kwa mama aliyeambukizwa.

(v) Kuwapa wanawake uwezo kiuchumi ili kuwawezesha akina mama kuwapatia watoto wao vyakula vya kulikiliza vyenye virutubisho.

## 5.15. Masuala ya Jinsia Kuhusiana na VIRUSI VYA UKIMWI/ UKIMWI

Nchini Tanzania njia kuu ya kueneza UKIMWI ni kwa kujamiiana baina ya watu wa jinsia tofauti. Hivyo, upo umuhimu wa kushughulikia masuala ya usawa kijinsia, na kuendeleza ushiriki sawa wa wanaume na wanawake katika kujadili njia salama za kujamiiana, na wanawake wana haki na wahamasishwe kusema HAPANA au kukataa kutumia njia isiyo salama.

Wanaume na wanawake wanapaswa kupewa hadhi sawa, fursa sawa za elimu, nafasi za elimu ya afya ya uzazi, na huduma za matunzo ya afya, uongozi na maendeleo katika nyanja zote. Ingawaje Sera za kuhusiana na mambo haya zipo, masuala ya VVU/UKIMWI yanahitaji utekelezaji wa sera katika shughuli za nyanja na viwango vyote.

(a) Uhusiano wa mamlaka katika shughuli za desturi na mila zinazozuia wanaume na wanawake kushiriki sawa katika kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI utashughulikiwa na sekta zote.

(b) Mila na desturi ambazo husaidia kuelimisha umma zitatumiwa kama kanuni za kutoa mamlaka na usambazaji wa Taarifa, Elimu na Mawasiliano (IEC) kuhusu afya ya uzazi, VVU/UKIMWI.

(c) Programu za jamii zitashughulikia masuala ya wenza/wapenzi zaidi ya mmoja katika kujamiiana na suala la haki za jinsia na uzazi kuhusiana na kuenea kwa maambukizo ya UKIMWI.

(d) Huduma za afya ya uzazi za uwiano, bora na zisizo na gharama zitatolewa kwa wanaume, wanawake na vijana.

(e) Sheria zilizopo za urithi zitapitiwa tena na kulinganishwa. Juhudi zitafanywa za kuzishawishi sheria na tabia za kimila zishughulikie pia masuala ya kijinsia.

# 6.0. KUPIMA UKIMWI

## 6.1. Madhumuni

Madhumuni makuu ni kueleza kwa ufasaha masharti ya maadili katika kupima UKIMWI kwa kuuchunguza ugonjwa, kuutibu, majaribio na utafiti wa hiari.

## 6.2. Kupima UKIMWI

(i) Kwa ajili ya upimaji wa hiari wa UKIMWI, ushauri nasaha wa kabla na baada ya kupima utafanywa ili kuwezesha mtu kupewa matokeo ya vipimo, na kama bado ni mdogo, kutolewa kwa wazazi au walezi. Shabaha kuu ni kuwathibitishia na kuwatia moyo asilimia 85-90 ya watu ambao hawana UKIMWI kuchukua hatua za uhakika za kutokuambukizwa, na wale ambao wana VVU kupewa msaada wa ushauri na matunzo vya kukabiliana na hali zao, kuongeza siku za kuishi na kutokuwaambukiza wengine.

(ii) Kwa upimaji ambao anayepimwa hatatambulika (unlinked HIV testing), ushauri nasaha wa kabla na baada ya kupima hautahitajika. Watu wanaojitolea kutoa damu ambao watapenda kujua matokeo ya vipimo vyao, taratibu zitawekwa za kufuatilia vipimo vya VVU vya hiari kwa ushauri nasaha kabla na baada ya upimaji.

## 6.3. Usiri

Vipimo vyote vya VVU vitakuwa ni siri. Hata hivyo, sheria za afya ya jamii zitawekwa ili kuwaamuru wataalamu wa afya kuamua kila jambo peke yake na kuzingatia maadili, kwa kuwafahamisha wapenzi wa wagonjwa kuhusu hali ya VVU ya wapenzi wao. Uamuzi kama huo utafanywa tu kulingana na vigezo vifuatavyo:

(i) Mtu mwenye VVU kushauriwa kwa ukamilifu.

(ii) Ushauri nasaha kwa mtu mwenye VVU umeshindwa kufikia mabadiliko ya tabia yanayofaa.

(iii) Mtu mwenye VVU amekataa kumtaarifu mwenzie, au kukataa kutoa kibali cha kumtaarifu mwenzie.

(iv) Hatari halisi ya uambukizo wa VVU kwa mwenzi/wenzie inaonekana.

(v) Mtu mwenye VVU anapewa taarifa ya awali mapema iwezekanavyo.

vi) Ufuatiliaji unafanywa ili kuhakikisha kuwa msaada unaotolewa kwa wanaohusika, ni lazima.

**idhaa ya kutoa taarifa**

i) Ridhaa ya kutoa taarifa baada ya ushauri nasaha wa kutosha itaombwa kwa mtu kabla upimaji wa VVU haujafanywa.

i) Wagonjwa waliolazwa hospitalini, au wagonjwa waliopoteza fahamu na wale wanaoonekana kwamba hawana akili timamu, hawataweza kutoa idhini ya kutoa taarifa. Ushauri nasaha utamhusisha ndugu wa karibu zaidi kutoa idhini kabla ya kuanza uchunguzi na matibabu.

**umtaarifu Mpenzi**

Iadaktari na Wafanyakazi wa afya hawaruhusiwi umuarifu mtu yeyote zaidi ya mtu aliyepimwa juu ya natokeo bila ya idhini yake. Ushauri utakazania jukumu a kuwaarifu wapenzi wote wawili na wenyendoa kwenda upima pamoja. Iwapo mtu aliyepimwa atakataa mtu eyote asifahamishwe, uamuzi wa kumfahamisha mtu wa atu utafuata masharti yaliyoelezwa katika fungu la 3.2 b) kuhusu Usiri. Wenza ambao hawatashiriki katika ıshauri pamoja na mtu aliyepimwa, watashawishiwa wenda kupewa ushauri kabla hawajafahamishwa kuhusu natokeo ya vipimo vya VVU vya mtu husika.

**umtia mtu hatiani kwa kosa la jinai kwa kuambukiza VU kwa makusudi**

wa kuzingatia kiwango kikubwa cha maambukizo ya VVU atika jamii, kanuni za adhabu zitarekebishwa kuwatia ıatiani kwa kosa la jinai wale ambao wataambukiza VVU wa wenzao kwa makusudi.

### 6.7. Kupima UKIMWI kabla ya ndoa

Upimaji wa VVU kabla ya ndoa utahimizwa na kuwezesha kufanyika kwake kwa gharama nafuu nchini kote. Kama ilivyo kwa vipimo vingine vyote utakuwa wa hiari kwa kupewa ushauri nasaha kabla na baada ya kupima.

### 6.8. Utafiti unaohusu Upimaji wa UKIMWI

Mapendekezo yote ya utafiti yatapata kwanza kibali kutoka kwenye Kamati ya Utafiti na Maadili ya Taasisi au Sekta mwenyeji husika. Tume ya Kudhibiti UKIMWI itafahamishwa kuhusu matokeo ya utafiti kwa ajili ya kumbukumbu na/au kwa ajili ya kuyasambaza. Mapendekezo ya utafiti yatakayoidhinishwa yatasajiliwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Utafiti utakaowahusisha washiriki wa kimataifa utapata kibali cha kimaadili kutoka kwenye Taasisi waliko washiriki wa kimataifa na pia kutoka kwenye Taasisi na Sekta zinazohusika za utafiti za Taifa. Waandishi wote watatoa ukubalifu kimaandishi, kwenye chapisho la ripoti ya utafiti.

### 6.9. Uchunguzi wa UKIMWI

Kwa madhumuni ya ufuatiliaji mwenendo wa mlipuko wa UKIMWI, kipimo chenye nguvu sana na mahususi kitapendekezwa kitumike kutegemeana na usahihi wa matokeo yanayotakiwa. Hata hivyo, uthibitisho unaweza kutumika kulingana na mahitaji ya utafiti na mahitaji mengine kama rufaa kwa kubainisha mapema vipimo na matibabu ya maambukizo yanayoambatana na ugonjwa.

### 6.10. Gharama za Vipimo vya UKIMWI

Watu wanaojitolea kwa hiari yao wenyewe wanaweza kutakiwa kuchangia gharama za ushauri na vipimo. Gharama za upimaji VVU hospitalini na katika vituo vingine vya upimaji zitategemea sera au kanuni za hospitali au kituo hicho.

### 6.11. Upimaji UKIMWI wakati wa Ujauzito

Huduma za ushauri na upimaji UKIMWI wa hiari zitaendelezwa na kutolewa kwa kina mama wajawazito kwa madhumuni ya kuzuia maambukizo ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto.

## UDUMA KWA WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA :IMWI /UKIMWI

### adhumuni

adhumuni makuu ni kuendeleza msaada wa lishe, kijamii ı kimaadili kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWIi ni ıwawezesha kuishi maisha mazuri, kuendelea kuzalisha a kuishi maisha marefu wakiwa na VVU/UKIMWI. Ni eneo ıalotoa changamoto ikizingatiwa kuwa bado hakuna ratibu na vyombo vinavyotoa misaada ya aina hiyo. Jamii, ashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), Mashirika ya ımuiya (CBOs), sekta binafsi na vikundi vya dini ni .uhimu sana katika kurahisisha juhudi hizi. Jinsi ambukizo unavyoshika kasi ndivyo kutakavyokuwepo na ıamia ya maelfu ya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI nbao watahitaji msaada.

ı) Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI watapewa fursa ya kupata matunzo ya afya kamili. Yakiwa ni pamoja na huduma za matibabu, ushauri nasaha na ustawi wa jamii. Matunzo ya afya hayatafanywa hospitali tu bali yatahusisha pia ruhusa zinazopangwa na mgonjwa kurejeshwa nyumbani kwa matunzo.

ɔ) Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI watapewa fursa ya kupatiwa ushauri nasaha pamoja na kupewa maelezo ya jinsi ya kuishi kwa matumaini na VVU/UKIMWI huku wakijikinga wao wenyewe na wengine wasiambukizwe.

:) Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI watakuwa na wajibu wa kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za jamii.

d) Watoaji wa matunzo katika taasisi na kijumuiya wana jukumu la kutunza watu walioambukizwa VVU bila ya ubaguzi kutokana na hali yao ya kuwa na VVU.

e) Taasisi zitatoa matunzo yaliyo bora kwa kuzingatia miongozo ya matunzo ya kitaasisi iliyopo na miongozo ya matibabu inayotolewa na serikali.

(f) Matunzo ya nyumbani na matunzo ya hospitali hukamilishana (complement each other). Kutakuwepo na mpango mkakati wa kuunganisha uhusiano huu unaokamilishana na bajeti ya kila kipengee katika halmashauri za mitaa.

## 7.2. Huduma za matunzo na msaada vinavyotolewa na Jamii.

Ukabilianaji unaohusisha vipengele vyote vya kudhibiti VVU/UKIMWI (comprehensive response) wa jumla umeonyesha kuleta mafanikio katika udhibiti wa UKIMWI. Huu unajumuisha uzuiaji, matunzo na msaada kwa wagonjwa wa UKIMWI katika jumuia ikiwa ni pamoja na huduma ya matunzo ya nyumbani. Hata hivyo ni lazima ifahamike kuwa katika ngazi ya kaya, utunzaji wa mgonjwa wa UKIMWI unagharimu sana kibinadamu, muda na kifedha. Msaada kutoka kwa jamii unahitajika sana.

(a) Serikali itaanzisha ushirikiano na watu binafsi, makampuni, mashirika au vyombo katika jamii vinavyoendeleza huduma za matunzo kwa wagonjwa na yatima wa UKIMWI.

(b) Serikali itahimiza ushirikiano na jumuiya za kidini katika kutoa matunzo ya kiroho na msaada wa vitu kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI. Malezi kiroho ni sehemu ya matunzo matakatifu.

(c) Madai yote kutoka kwa umma ya uwezo wa kutibu VVU/UKIMWI kwa tiba za jadi, au za kidini au ya watabibu wengine yasitiliwe maanani kwanza mpaka yathibitishwe na kuidhinishwa na taasisi za Serikali.

(d) Uingizaji kutoka nje na utengenezaji wa dawa za kisasa na za jadi za kutibu VVU/UKIMWI utaendelezwa na kuidhinishwa na taasisi za kiserikali.

(e) Serikali itahimiza majaribio ya haraka ya madawa na usajili wa dawa za kisasa na za jadi za tiba ya UKIMWI.

(f) Mbinu za kuanzisha Mfumo Maalumu kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za jamii katika kuwasaidia na kuwatunza walioambukizwa na kuathiriwa na VVU/UKIMWI zitaanzishwa.

**nga kwa Watoa Huduma za Afya na Wakunga wa Jadi**

'a kuzingatia kuenea kwa VVU/UKIMWI kwa kiwango :ubwa katika jamii, watoa huduma za afya na wakunga jadi wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa VVU toka kwa wagonjwa wakati wanapotekeleza majukumu ). Kwa hiyo lengo kuu ni kuwapa mamlaka watoa duma za afya na wakunga wa jadi kuchukua hadhari ya ambukizwa na kuhakikisha kuwa taasisi zinazotoa duma za afya wanatoa vifaa vya kujikinga kwa fanyakazi kulingana na kanuni za hadhari za kinga dhidi magonjwa na vitu vya kuambukiza.

Watoa huduma za afya watapewa mafunzo ya kujikinga binafsi dhidi ya UKIMWI na kuzuia kuenea kwake kunakotokea wakati wa kugusana na damu, majimaji ya mwili, viungo na tishu. Mafunzo kuhusu kinga binafsi yatatolewa kwa wakunga wa jadi.

Taasisi zote zinazotoa huduma za afya zitatoa vifaa vya kinga kwa watoa huduma vituoni na nyumbani na kwa wakunga wa jadi.

Huduma za ushauri na msaada muhimu katika kushughulikia waathirika zitaanzishwa kwa watoa huduma.

**uduma za Msaada**

/U/UKIMWI ni tatizo la kijamii, kitamaduni na kiuchumi nbalo limeweka wazi masuala mengi kijamii, utamaduni, kisheria, kijinsia na haki za binadamu ıhusiana na ustawi wa idadi kubwa ya wajane na yatima anaotokana na vifo vinavyosababishwa na UKIMWI. adhumuni makuu ya huduma za msaada ni kuanzisha fumo kisheria na kijamii wa kuendeleza huduma na saada kwa waathirika wa VVU/UKIMWI. Juhudi nazofanywa na sekta mbalimbali zitaendelezwa ili ıhimiza ueleo na kukubalika kufaao kwa VVU katika jamii VVU/UKIMWI ukubalike kama magonjwa mengine ya nadamu. Halmashauri za serikali za mitaa na jumuiya ı mtaa zitasaidiwa kuendeleza huduma za msaada kwa atu wanaoishi na VVU/UKIMWI, wajane na yatima katika .muiya zao.

.) Serikali itahimiza na kuendeleza ushiriki wa sekta mbalimbali katika kuielimisha jamii kuhusu sheria

zilizopo, ambazo zinatetea haki za wategemezi walio hai, na itahakikisha kuwa wanapewa haki zao za kurithi ardhi na mali za marehemu. Jamii itashirikishwa katika kuhakikisha kuwa huduma na msaada vinatolewa kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, wajane na yatima.

(b) Serikali itahakikisha kuwa Sera za sekta zote zinazungumzia haki za wategemezi walio hai.

(c) Msaada na kinga muhimu dhidi ya VVU/UKIMWI vitatolewa kwa yatima na watoto katika taasisi mahususi wakiwemo watoto wa mitaani na wale wasiojiweza ambao wako katika hatari ya kuambukizwa VVU.

(d) Yatima kutoka kaya moja watahitaji msaada kutoka Serikali Kuu na Halmashauri za Serikali za mitaa na jamii ili kupunguza athari za matokeo (impact) ya UKIMWI katika maisha yao. Msaada kama huo utazingatia haki za watoto.

(e) Maana ya yatima, katika muktadha wa jamii ya Kitanzania kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI, ni mtoto kati ya umri wa miaka 0-15 ambaye amepoteza wazazi wake wote wawili.

## 'ITI

### ɬadhumuni

ɬadhumuni makuu ni kuweka mfumo wa kuendeleza na ‹uratibu shughuli za utafiti za sekta mbalimbali na nyanja nbalimbali katika VVU/UKIMWI, kusambaza na kutumia natokeo ya utafiti. Hili ni baada ya kuona kwamba UKIMWI ımesababisha mambo mengi mazito ambayo yanahitaji ɔrogramu za utafiti zinazogharimiwa na kuratibiwa .pasavyo.

a) Utafiti kuhusu harakati za kisayansi na kimaadili katika UKIMWI na ambao utawezesha kuongeza maarifa mapya ambayo ni muhimu, yanayofaa na kutumiwa na jamii utahimizwa.

b) Miundo ya utafiti iliyopo itatumiwa katika utafiti wa VVU/UKIMWI

c) Utafiti kuhusu VVU/UKIMWI unaohusu masuala ya binadamu, utazingatia Sheria ya Madaktari wa kawaida na wa Meno na Miongozo ya Kitaifa ya Utafiti wa Elimu ya Tiba. Utafiti wa Saikolojia ya Jamii na Sayansi Jamii utafuata miongozo ya maadili ya kazi iliyowekwa.

d) Serikali itaanzisha mikutano ya kuchangia na kushirikishana taarifa za kisayansi na kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanaweza kutolewa na kupatikana kwa urahisi.

### ɾaratibu za Utafiti kuhusu VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI

a) Kutakuwepo na Kamati ya Taifa ya Utafiti na Maadili itakayoshughulikia masuala ya VVU/UKIMWI. Kamati hii itajumuisha wawakilishi kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Sekta za Utafiti kuhusu UKIMWI, COSTECH, NIMR, Vyuo Vikuu, Wizara ya Sheria, na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs).

b) Utafiti kuhusu UKIMWI utakaohusisha watafiti wa Kimataifa utatakiwa kupata kibali cha Kamati ya Taifa ya Utafiti na Maadili kuhusu UKIMWI na itakuwa na mshiriki mwingine mwandamizi wa kitaifa ambaye atawajibika na utafiti nchini.

(c) Kibali cha utafiti wa UKIMWI kitatolewa na Kamati za Taasisi za Utafiti na Maadili zilizopo na kuidhinishwa na mamlaka husika.

(d) Watafiti wote wa UKIMWI watawasilisha nakala za taratibu za tafiti zao na hati za vibali kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa ajili ya kumbukumbu.

## 8.3. Vipaumbele vya Utafiti wa Taifa kuhusu VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI

(a) Vipaumbele vya Utafiti vitatayarishwa ili kuruhusu kupatikana kwa haraka kwa maarifa, mambo muhimu na taarifa kuhusu VVU/UKIMWI.

(b) Kamati ya Taifa ya Utafiti na Maadili ya UKIMWI itapitia upya na kuvirekebisha mara kwa mara vipaumbele vya utafiti vya Taifa kuhusu UKIMWI.

## 8.4. Usambazaji wa Matokeo ya Utafiti

(a) Sekta zote zitaweka orodha ya miradi yote ya utafiti kuhusu VVU/UKIMWI inayoendelea na iliyokamilishwa kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI ambayo itatayarisha orodha na kusambaza matokeo muhimu ya utafiti kwa washika dau wanaohusika.

(b) Watafiti watatafsiri matokeo ya utafiti katika lugha inayoeleweka kwa ajili ya kutumiwa na umma.

## 8.5. Ugharimiaji wa Utafiti wa UKIMWI

(a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itatafuta fedha kwa ajili ya uratibu na uendelezaji wa shughuli za utafiti, na usambazaji wa matokeo ya utafiti.

(b) Taasisi zinazofanya utafiti na watu binafsi watatafuta ruzuku zao wenyewe na aina yoyote ile ya msaada unaohusiana na utafiti.

(c) Kila sekta itajitahidi kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli za utafiti wa UKIMWI.

# SURA YA 9

## A ZA SEKTA NA UGHARIMIAJI

### adhumuni

(IMWI ni tatizo la Kitaifa linaloathiri Sekta zote katika 'anja zote. Kwa hiyo lengo kuu ni kuendeleza mkabala wa sekta ulioratibiwa vizuri na unaofaa katika kukabiliana ı ugonjwa huu wa mlipuko na kutafuta fedha za kutosha va ajili ya shughuli za VVU/UKIMWI. Dhima za sekta neainishwa kwenye miongozo ya Sera ya Taifa ya shirikishwaji wa Sekta mbalimbali kuhusu VVU/UKIMWI

.) Serikali kuu na Serikali za Mitaa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali/Mashirika ya Jumuiya, Mashirika ya Kidini na Sekta na Taasisi Binafsi vitapanga na kutekeleza shughuli za masuala ya UKIMWI katika Sekta zao.

ı) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itakuwa na wajibu mkubwa wa kuzisaidia sekta mbalimbali katika kupanga, kutekeleza na kutathmini jinsi ya kuzuia na kudhibiti UKIMWI na kupunguza athari zake.

:) Sekta mbalimbali kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI itapanga Mpango Mkakati wa Taifa kwa ajili ya udhibiti VVU/UKIMWI ndani ya mfumo unaoshirikisha sekta mbalimbali ili kukabiliana na ugonjwa huu.

l) Ndani ya mfumo wa Mpango Mkakati wa Taifa wa UKIMWI, kila sekta itapanga bajeti yake, kuchangisha fedha na kutafuta vifaa na watu kwa ajili ya shughuli zake za kudhibiti UKIMWI.

:) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itasaidia katika kutafuta fedha na itawajibika na tathmini ya mara kwa mara ili kujua matokeo ya fedha za wafadhili wa ndani na nje katika kuzuia na kudhibiti UKIMWI.

) Ndani ya Mfumo wa Mpango mkakati kila sekta itaainisha, kutoa vipaumbele vyake na kutekeleza shughuli za kinga na udhibiti wa UKIMWI sambamba na uwezo na manufaa yake.

;) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itapanga mbinu za kuanzisha Mfuko wa UKIMWI ambao utapata fedha kutoka Serikalini na kwa washika dau na watu binafsi kwa ajili ya kusaidia harakati za jamii.

## SURA YA 10

## .0.0. MUUNDO NA UENDESHAJI WA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI (TACAIDS)

### 10.1. Utangulizi

Uendeshaji na Usimamizi wa Programu ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya sekta mbalimbali utazingatia marekebisho yanayoendelea nchini. Utahitaji pia kutambua hali ngumu ya kudhibiti janga la UKIMWI kutokana na jinsi UKIMWI unavyokuwa na sura na maingiliano mengi katika nyanja mbali mbali ya maisha ya jamii. Tume ya Kudhibiti UKIMWI ina wajibu wa kutekeleza Sera hii kama ilivyotajwa kwenye sura ya I mpaka II.

### 10.2. Dira

Dira ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ni: -

Kuwa na jamii ambamo watoto wetu wanaweza kukua bila ya tishio la Virusi vya UKIMWI/UKIMWI na ambayo inawajali na kuwasaidia wale ambao wameambukizwa na kuathiriwa na VVU/UKIMWI.

### 10.3. Jukumu Maalum

Jukumu maalum la Tume ya Kudhibiti UKIMWI ni: -

Kuandaa uongozi mkakati kwa sekta mbalimbali za kitaifa kukabiliana na VVU/UKIMWI ambao utasaidia kupunguza kuenea zaidi kwa maambukizo ya VVU na magonjwa yanayoambatana na UKIMWI na athari mbaya za UKIMWI katika uchumi wa jamii.

### 10.4. Lengo

Lengo la Tume ya Kudhibiti UKIMWI ni: -

Kuratibu utekelezaji wa shughuli za sekta mbalimbali za kitaifa kukabiliana na VVU/UKIMWI.

### 10.5. Madhumuni

Jukumu hili maalum limefafanuliwa katika madhumuni manane makuu:

(a) Kuweka mfumo wa kimkakati na miongozo ya taifa kusaidia katika kupanga, kuratibu na kutekeleza shughuli za Sekta mbalimbali za kukabiliana na VVU/UKIMWI katika ngazi zote.

b) Kuendeleza na kuwezesha utekelezaji wa mkakati wa taifa wa kukusanya na kutumia raslimali kwa ajili ya VVU/UKIMWI.

c) Kuendeleza na kuwezesha utekelezaji wa mkakati wa taifa kwa ajili ya uraghibishi kuhusu VVU/UKIMWI.

d) Kuanzisha na kukuza ubia ili kuongeza muitiko miongoni mwa washika dau, k.v. Taasisi za Serikali, Wabia wa Kimaendeleo, Serikali, Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI/UKIMWI, Sekta Binafsi, Mashirika ya Kiserikali (NGOs), Taasisi za Dini, Mashirika ya Jumuiya (CBOs) na Mashirika ya Umma.

e) Kuendeleza utafiti kuhusu UKIMWI na kukuza uhusiano na taasisi nyingine za utafiti.

f) Kuanzisha na kuendeleza mfumo wa usimamizi wa taarifa za VVU/UKIMWI wa Sekta mbalimbali na kurahisisha usambazaji wa taarifa.

(g) Kuanzisha mfumo madhubuti utakaofuatilia mwelekeo wa UKIMWI na jinsi taifa zima linavyokabiliana na VVU/UKIMWI.

(h) Kuanzisha na kuendeleza ufanisi na uwezo wa usimamizi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI.

**Kazi za Tume**

(a) Kuweka miongozo ya Sera kwa ajili ya kukabiliana na VVU/UKIMWI na kusimamia matokeo yake katika Tanzania Bara.

(b) Kuanzisha mfumo mkakati kwa ajili ya kupanga programu na shughuli zote za udhibiti wa VVU/UKIMWI ndani ya mkakati mzima wa taifa.

(c) Kuhimiza umoja wa kitaifa na kimataifa miongoni mwa washikadau kwa uratibu unaofaa wa programu na shughuli zote za udhibiti wa VVU/UKIMWI ndani ya mkakati mzima wa taifa.

(d) Kukusanya, kulipa na kufuatilia raslimali na kuhakikisha zinasambazwa kwa usawa kadri iwezekanavyo.

(e) Kusambaza taarifa za VVU/UKIMWI na matokeo yake katika Tanzania kuhusu programu kwa ajili ya udhibiti wake.

(f) Kuendeleza utafiti, ushirikianaji habari na uhifadhi wa nyaraka zinazohusu VVU/UKIMWI.

[g] Kukuza viwango vya hali ya juu vya uraghibishi na elimu kuhusu kinga na udhibiti wa VVU.

(h) Kufuatilia na kutathmini shughuli zote zinazoendelea kuhusu VVU/UKIMWI.

(i) Kuratibu shughuli zote zinazohusiana na usimamizi wa masuala ya VVU/UKIMWI nchini Tanzania kulingana na mkakati wa taifa.

(j) Kusaidia juhudi za kutafuta chanjo, tiba, urahisi wa kupata matibabu na matunzo.

(k) Kutetea haki za binadamu za walioambukizwa na waathirika wa VVU/UKIMWI.

(l) Kuhimiza hali ya kuishi vizuri kwa matumaini miongoni mwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

(m) Kuishauri Serikali kuhusu masuala yote yanayohusiana na udhibiti wa UKIMWI.

## 10.7. Sera

(a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itapewa mamlaka yanayofaa na uwezo kisheria wa kutekeleza majukumu na kazi zake kama zilivyotajwa hapo juu.

(b) Tume ya Kudhibiti UKIMWI iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu itasaidia sekta mbalimbali za kitaifa katika juhudi zake za kupambana na VVU/UKIMWI

(c) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itakuwa na utaratibu madhubuti na watumishi wa kuratibu jitihada za sekta mbalimbali katika ngazi zote.

(d) Tume ya Kudhibiti UKIMWI itapewa uwezo wa kukuza ushirikiano na ubia katika shughuli za VVU/UKIMWI kitaifa na kiulimwengu.